HOTUBA YA MSTAHIKI MEYA MHE. RENATUS BAHEBE MULUNGA WAKATI WA MKUTANO WA KWANZA WA BARAZA LA MADIWANI ILEMELA, 2 DESEMBA, 2020

i. MHE.MWENYEKITI WA CCM (W) YA ILEMELA

ii. WAHE.WAJUMBE WA KAMATI YA SIASA YA CCM (W) YA ILEMELA

iii. MHE. MKUU WA WILAYA YA ILEMELA,

iv. MHE. MBUNGE WA JIMBO LA ILEMELA

v. WAHE. WAJUMBE WA KAMATI YA USALAMA YA WILAYA YA ILEMELA

vi. WAHE. WAJUMBE WA BARAZA LA MADIWANI WA HALMASHURI YA MANISPAA YA ILEMELA

vii. WAHESHIMIWA VIONGOZI WA KAMATI YA AMANI YA WILAYA YA ILEMELA (VIONGOZI WA DINI)

viii. MHE.KATIBU TAWALA WA WILAYA YA ILEMELA

ix. MKURUGENZI NA WATENDAJI (WATUMISHI) WOTE WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA[IKIWA PAMOJA NA WARATIBU ELIMU KATA, WALIMU WAKUU NA WAKUU WA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI]

x. WENYEVITI WOTE WA SERIKALI ZA MITAA 171 YA HALMASHAURI YA MANIPSAA YA ILEMELA

xi. WAANDISHI WA HABARI KUTOKA VYOMBO VYOTE TELEVISHENI NA MAGAZETI.

xii. MABIBI NA MABWANA.

ASALAM ALYEKUM, BWANA YESU ASIFIWE, TUMSIFU YESU KRISTU.

Awali ya yote, napenda nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia neema ya uzima, kwa kutuwezesha kuiona siku hii ya leo. Vilevile, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania- Dkt.John Pombe Joseph Magufuli yeye pamoja na Makamu wa Rais kwa kuchaguliwa kwao kwa kura nyingi kuliongoza Taifa letu kwa kipindi kingine cha miaka mitano 2020-2025.

Aidha, nampongeza Mhe. Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Dkt. Angeline S.L.Mabula kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Ilemela kwa kura nyingi kuwa mwakilishi wa wananchi kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Nawapongeza pia wahe. Madiwani wenzangu tuliochaguliwa na wanachi katika maeneo ya kata zetu kwa kura nyingi kuzidi wagombea wa vyama rafiki.Hongereni sana waheshimiwa madiwani kwa kuwa na Baraza linaloongozwa na Chama cha Mapinduzi.Huu ni uthibitisho tosha kwamba, Wananchi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela wamekiamini Chama cha Mapinduzi kupitia uongozi madhubuti wa mwenyekiti Mhe. John Pombe Joseph Magufuli kwa kukipatia ushindi mkubwa wa kishindo kwa nafasi zote tatu (yaani Urais, ubunge na madiwani). Hivyo, ni rai yangu tusiipoteze imani hiyo waliyotupa, badala yake tufanye kazi kadri ya nguvu na maarifa aliyotujalia mwenyezi Mungu, kwa sababu uwezo na nia ya kuwatumikia tunao.

Nitumie fursa hii kukishukuru Chama changu cha CCM kunipitisha kugombea nafasi hii na kisha ninyi wajumbe wa Baraza hili kunichagua kuwa Mstahiki Meya wa Halmashauri yetu.Nawashukuru sana.

Nitumie fursa hii pia kumpongeza Mhe. Manusura Sadick Lusigaliye kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi na kisha kuchaguliwa na ninyi Wajumbe kuwa Naibu Mstahiki Meya wa Halmashauri yetu.

Kwa moyo dhati naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru viongozi wetu wa madhahebu ya dini zote zilizomo katika eneo la Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa namna mnavyoshirikiana nasi katika utekelezaji wa majukumu yetu. Ninawaomba muendelee kutuombea sisi Waheshimiwa Madiwani pamoja na wananchi wote ili Halmashauri yetu iendelee kubaki katika mikono ya mwenyezi mungu.

Ndugu wananchi na Wajumbe wa Baraza la Madiwani kwa namna ya pekee nampongeza Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela Bw. John Paul Wanga pamoja na Timu yote iliyosimamia Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 Mwaka 2020 kwa namna walivyosimamia uchaguzi. Hakika kazi yao ilikuwa nzuri, kwasababu katika kipindi chote cha mchakato hapakuwa na dosari zozote za kiuchaguzi ambazo zingeweza kusababisha malalamiko au manung'uniko

toka kwa Wagombea, Mawakala wao, Wapiga kura pamoja na wafuasi na/au wananchi na hata kuathiri uchaguzi. Jimbo letu la Ilemela lilikuwa shwari na salama wakati wote, kiasi cha kuwafanya wananchi kuitumia haki yao ya kikatiba bila bughudha yoyote. Hongereni sana kwa kazi nzuri.

Niwaombe Waheshimiwa Madiwani na Wananchi wote wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, uchaguzi sasa umeisha ni jukumu letu sote kuchapa kazi ili kuwaletea maendeleo wananchi ikiwa ni pamoja na kuinua uchumi wa Halmashauri yetu na Taifa kwa ujumla.

Mhe.Mwenyekiti wa Mkutano huu, ninaomba nitoe Hotuba yangu katika Mkutano wa Kwanza wa Baraza la Madiwani kwa kuanisha muelekeo wa Halmashauri yetu katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2020-2025).

Utekelezaji wa majukumu yetu utazingatia Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama cha Mapinduzi [2020-2025] pamoja na vipaumbele vya Serikali ya awamu ya tano.

Pamoja na malengo tuliyokuwa nayo katika kipindi cha awamu ya kwanza ya awamu ya tano [2015-2025] Halmashauri yetu, itaendelea kutekeleza malengo hayo sambamba na yale yaliyoanishwa katika Ilani na vipaumbele vya serikali.Kwa ujumla yapo ambayo tumefanikiwa kutekeleza japo si kwa kiwango cha kumaliza kabisa changamoto,katika sekta ya miundo mbinu ya barabara, afya, elimu, maji, nishati, ukusanyaji wa mapato,uwezeshaji wananchi kiuchumi na utawala bora.

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo tunakusudia kuendelea kuisimamia Halmashauri kwa kuweka msukumo katika maeneo yafuatayo:-

1.0 UTAWALA BORA

Katika kuzingatia misingi ya Utawala Bora kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Taifa kwa ujumla, Halmashauri tutahakikisha tunatekeleza yafuatayo**:-**

i. Kujenga jamii yenye ari na uhuru wa kujituma na kushiriki katika masuala ya maendeleo na kisiasa kwa kuzingatia maadili na Sheria za Nchi.

ii. Kusimamia nidhamu, uadilifu, uwazi na uwajibikaji miongoni mwa Viongozi, Watumishi wa Umma wa Halmashauri.

iii. Kujenga jamii inayoheshimu na kuthamini utu, usawa na haki mbele ya Sheria katika kujiletea maendeleo.

iv. Kuendelea kuiomba Serikali kuongeza watumishi katika maeneo yote yenye upungufu.

v. Kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi kwa wakati, kwa haki na uadilifu kwa kuondoa urasimu usiokuwa wa lazima.

vi. Kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ili kuongeza uwezo wa Halmashauri kutoa huduma kwa wananchi kutoka kiwango cha Tsh. 9,835,947,990.00 mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kiwango cha Tsh. 19,286,172,529.00 ifikapo mwaka wa fedha 2024/2025.

vii. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato pamoja na maeneo ya sekta zingine ambazo zinatumia mifumo ya kielektroniki.

viii. Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kupata tija na ubora kulingana na thamani ya fedha iliyotumika *(value for money).*

Vile vile, katika eneo la utawala bora, Halmashauri itahakikisha waheshimiwa madiwani wanakuwa kioo kwa wananchi wanaowaongoza kwa kuhakkisha wanashiriki kikamilifu katika kuhamasisha shughuli za maendeleo bila kukwamisha utekelezaji wa maazimio na/au maelekezo ya serikali.Aidha, tutaendelea kusimamia utekelezaji wa Ahadi za Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli alizotoa kwa upande wa Wilaya ya Ilemela zinatekelezwa ifikapo mwaka 2025 kupitia Mhe. Mbunge wa Jimbo la Ilemela.

2.0 Ukusanyaji wa mapato ya halmashauri na serikali kuu

Kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ili kuongeza uwezo wa Halmashauri kutoa huduma kwa wananchi kutoka kiwango cha Tsh. 9,835,947,990.00 mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kiwango cha Tsh. 19,286,172,529.00 ifikapo mwaka wa fedha 2024/2025.

Katika ukusanyaji wa mapato ya halmashauri na serikali kuu kwa maana ya kodi ya majengo, kodi ya pango la ardhi n.k.

Vilevile, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, tutaendelea kubuni njia rahisi yenye gharama nafuu katika kukusanya na kusimamia mapato. Aidha, tunaipongeza serikali ya awamu ya tano kwa kuendelea kuhimiza matumizi ya mifumo ya kukusanya mapato.Tunakamilisha utaratibu wa wa kuwaingiza katika mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za taarifa za kaya kwa kuwatumia mabalozi. Utaratibu huu tayari unatekelezwa na watumishi wa mifumo wa Halmashauri baada ya kupata mafunzo ya Geographical Information System (GIS) huko Kigoma.utajulikana kama "Balozi system", nina imani tutafanikiwa kuhakikisha kila mkazi wa halmashauri hii anachangia maendeleo kwa kulipa kodi.

3.0 USAFI NA UZOAJI TAKA

Tutaendelea kuimarisha mfumo wa usimamizi wa taka ngumu katika eneo letu la mji.natambua zipo changamoto za mrundikano wa taka ngumu zinazotoka katika makazi na biashara katika vituo vya kukusanyia taka. Tutahakikisha changamoto hizi tunazipatia ufumbuzi wa kudumu kwa kuwekeza katika vifaa na magari.

4.0 SEKTA YA MIUNDOMBINU

Katika Sekta ya miundo mbinu tutaendelea kuhakikisha miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi inaboreshwa ifikapo 2025, Halmashauri kwa kushirikia na TARURA itatekeleza yafuatayo**:-**

i. Kuongeza mtandao wa barabara kutoka 70% mwaka 2020 hadi 80% mwaka 2025.

ii. Kuongeza kiwango cha barabara za changarawe kutoka 65% mwaka 2020 hadi 75% mwaka 2025.

iii. Kuongeza urefu wa barabara za mijini na maeneo ya pembezoni zilizojengwa kwa kiwango cha lami kutoka 10% mwaka 2020 hadi 25% mwaka 2025 ambapo mipango wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara za Buswelu-Busenga-Cocacola kilometa 3.25, Mbogamboga – Nyamadoke – Nyamhongolo kilometa 9.25, Kahama – Shibula - Tx, – Igombe – Kayenze kilomita., Ilaila-Kabusungu-Sangabuye kilomita

42 na Pasiansi-Lumala-Kiseke PPF kilometa 3.25 inaendelea kwa hatua mbalimbali za utekelezaji wa awali, kama vile, manunuzi ya upembembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa michoro ya barabara hizo.

iv. Kusimamia utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati inayoendelea kujengwa ambayo ni mradi wa stendi ya mabasi na maegesho ya malori Nyamhongolo miradi hii kwa sasa imefikia asilimia 65 ya utekelezaji.

v. Kusimamia utekelezaji wa miradi mipya itakayotekelezwa na Serikali kwa ushirikiano na Benki ya Dunia ambayo ni Soko Kuu la Kisasa Kirumba, Barabara za kiwango cha lami za Buswelu-Busenga-Cocacola na Mbogamboga-Nyamadoke-Nyamhongolo pamoja na mradi wa ujenzi wa mifereji mikubwa ya kutiririsha maji ya mvua katika mto Kirumba.

5.0 SEKTA YA ELIMU

Katika kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi zote ifikapo 2025, Halmashauri itatekeleza mambo yafuatayo:-

i. Kujenga vyumba vya madarasa 300, vyumba vya Maabara za Sayansi 17, matundu ya vyoo 1000 na nyumba za Walimu 10 ambapo kwa sasa kuna madarasa 1006, vyumba vya maabara za sayansi 69, matundu ya vyoo 1234 na nyumba za walimu 178.

Vilevile, tutaanzisha shule mpya 5 za msingi na 5 za sekondari katika maeneo ya Kata ya Kahama, Shibula, Nyamhongolo, Buswelu,Bugongwa, Sangabuye na Kayenze ili kukabiliana na upungufu wa miundo mbinu ya wanafunzi kujifunzia.

ii. Kuimarisha miundombinu ya shule za sekondari Sangabuye, Buswelu na Kayenze kwa ajili ya kidato cha tano na sita.

iii. Kushirikiana na sekta binafsi, asasi za kiraia zikiwemo taasisi za dini kwa kutoa fursa za upatikanaji wa elimu.

iv. Kuimarisha misingi ya elimu ya kujitegemea, kuanzisha elimu ya kujitegemea (EK) ya bustani za mbogamboga na kilimo cha mazao ya chakula kwa shule zenye maeneo.

v. Tutaendelea kusimamia mpango wa serikali wa kutoa Elimu Bila Malipo kwa shule za msingi na sekondari kwa kuhakikisha fedha zinazotolewa na Serikali zinafanya kazi iliyokusudiwa.

vi. Tutaendelea kuhimiza na kufanya ufuatiliaji kwa Kuhakikisha kuwa shule za Msingi zote zilizomo katika Halmashauri yetu zinaaznisha madarasa na zinatoa elimu ya awali kwa ufanisi.

vii. Kupitia kamati ya huduma za jamii, afya na elimu tutaendelea kuimarisha ufundishaji wa masomo ya sayansi yakiwemo Hisabati, Fizikia, Kemia na Baiolojia na kuongeza upatikanaji wa walimu wakufundisha masomo hayo na watalaam wengine kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu.

viii. Tutaendelea kuiomba serikali kuongeza idadi ya walimu wa masomo ya masomo ya sayansi ili kuongeza nafasi za wanafunzi wanaosoma masomo ya Sayansi na Hisabati hususan watoto wa kike.

6.0 SEKTA YA AFYA

Katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya na siha bora ifikapo 2025, Halmashauri itasimamia yafuatayo:-

i. Kuimarisha huduma za afya ya Mama na Mtoto na kuzitoa bila malipo ili kupunguza vifo vya akinamama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

ii. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba, vifaa saidizi na vitendanishi katika vituo vyote vya kutolea huduma ya afya.

iii. Kuhamasisha jamii umuhimu wa matumizi ya vyandarua 600,000 vilivyowekwa dawa na upuliziaji wa viatilifu ukoko katika kuta za nyumba.

iv. Kutoa elimu ya kupambana na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukizwa

v. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya.

vi. Kujenga zahanati mpya 4 katika mitaa ya Nyamadoke, Masemele, Lumala na Bezi, kujenga vituo vipya vya afya 3 katika kata za Buswelu, Kayenze na Kiseke pamoja na kujenga Chuo cha Afya katika eneo la Hospitali ya wilaya.

vii. Kupunguza idadi ya watoto chini ya miaka mitano wenye udumavu

IMC

na ukondefu kwa kuhimiza kilimo cha mbogamboga ili kupata lishe bora.

viii. Kuwajengea uwezo wataalam wa afya ili watoe huduma za afya na lishe kikamilifu.

ix. Kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya VVU na UKIMWI ili kupunguza maambukizi na unyanyapaa hatimaye kuongeza nguvu kazi katika uzalishaji mali.

x. Kuimarisha kamati ya kuthibiti UKIMWI na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya huduma za UKIMWI ili kubaini changamoto.

xi. Tutaendelea kuimarisha huduma za matibabu bila malipo kwa wazee wa umri wa miaka sitini na kuendelea, sambamba na kuhakisha madirisha ya wazee yanafanya kazi katika vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya.

xii. Aidha, tutaimarisha mabaraza ya wazee katika Kata 19 ili kuwawezesha kubaini changamoto zinzzowakabili.

xiii. Kuendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na matibabu ya bima ya afya kupitia mpango wa iCHF hadi kufikia wanachama 45,000 ifikapo mwaka 2025 kutoka idadi ya wananchama 10,327 mwaka 2020.

xiv. Kuboresha rejista ya watu wenye ulemavu itakayotoa taarifa sahihi, kubuni na kutekeleza mikakati ya kuwawezesha kiuchumi watu wenye ulemavu na kujenga miundombinu rafiki ili kuhakikisha watu wenye ulemavu waweze kufikia huduma kirahisi.

7.0 SEKTA YA ARDHI

Katika kuendeleza rasilimali ardhi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii ifikapo 2025, tutatekeleza yafuatayo:-

i. Tutaendelea Kukamilisha kupanga na kupima ardhi yote ya Manispaa ya Ilemela kwa kuzingatia mpango kabambe wa Jiji la Mwanza wa mwaka 2015 – 2035.

ii. Kuendelea kuhifadhi taarifa za wananchi katika mfumo wa kierektroniki ili kurahisha mawasiliano baina ya Halmashauri na wamiliki wa ardhi kwa ajili ya kuboresha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ardhi na kuongeza kiwango cha mapato kutoka

5,100,000,000.00 mwaka 2020 hadi 9,225,806,451.60 mwaka 2025.

iii. Tutaendelea na ukamilishaji wa maeneo yaliyofanyiwa urasimisha ji ardhi iliyo kuwa inamilikiwa kimila na makazi yasiyo rasmi mijini ili kuwawezesha wamiliki wa ardhi kunufaika kwa kupata usalama wa milki kwa wananchi kupatiwa hati milki.

iv. Kumilikisha na kusajili vipande vya ardhi vipatavyo 500,000 na kutoa Hati miliki 520,000 ifikapo mwaka 2025.

v. Kulinda na kuyaendeleza maeneo ya Ihalalo na Nyamhongolo kwa ajili ya uwekezaji kulingana na Mpango kabambe wa Jiji la Mwanza.

vi. Kupima maeneo yote ya fukwe za ziwa viktoria ili kuyalinda kwa ajili ya uwekezaji wa miundombinu ya utalii kwa siku za mbeleni.

8.0 SEKTA YA MALIASILI

Katika kuimarisha usimamizi na uhifadhi maliasili ifikapo 2025, Halmashauri itatekeleza yafuatayo**:-**

i. Kutengeneza mizinga 500 na kuigawa kwa vikundi 4 vya wafugaji nyuki maeneo ya Sangabuye na Bugongwa.

ii. Kuendeleza program ya upandaji miti kutoka hekta 1,500 hadi 2,000 Mwaka 2025.

iii. Kulinda na kuimarisha fukwe za ziwa viktoria ili zisitumike holela kwa ajili ya kuvutia uwekezaji katika utalii.

9.0 SEKTA YA MAJI

Katika kuhakikisha huduma ya maji inawafikia zaidi ya asilimia 85 ya wakazi wa mitaa na zaidi asilimia 95 kwa mijini ifikapo 2025, Halmashauri itasisitiza yafuatayo**:-**

i. Kwa kushirikiana na Mamlaka ya maji na usafi wa mazingira Mwanza(MWAUWASA), Halmashauri itahakikisha ukamilishaji wa miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa na serikali kuhakikisha mitaa yote inayopitiwa na miradi hiyo inapata huduma ya maji safi na salama katika kata za Bugogwa, Shibula, Buswelu, Kahama na Nyamhongolo.

ii. Kuhamasisha ujenzi wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua

katika majengo ya Serikali, asasi za umma na nyumba za watu binafsi pamoja na uchimbaji wa visima.

iii. Tutaendelea kushirikiana na Mhe. Mbunge wa Jimbo la Ilemela katika maeneo mengine ambayo hayaguswi na miradi inayosimamiwa na MWAUWASA katika kutatua changamoto ya maji kupitia wadau wa Maendeleo kama ambavyo tumefanya katika awamu iliyopita.

10.0 SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA

Katika kujenga Uchumi wa Viwanda, Halmashauri tutaendelea**:-**

i. Kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo ili kunufaika na Mpango wa Kusambaza Umeme Vijijini–REA na kuongeza idadi ya viwanda vidogo vidogo kutoka 298 Mwaka 2020 hadi 500 Mwaka 2025.

ii. Kutenga maeneo maalum ya viwanda vya kati na vikubwa ili kuongeza idadi kutoka ya viwanda 11 Mwaka 2020 hadi 30 Mwaka 2025

iii. Kutenga na kuendeleza maeneo maalum ya uwekezaji (EPZ) ambapo Halmashauri itaendeleza mpango wa utekelezaji wa eneo maalum la uwekezaji Nyamhongolo.

iv. Kuweka mazingira wezeshi ya biashara na kuhakikisha zinapatikana fursa nafuu za kibiashara kwa kuboresha miundombinu ya biashara iliyopo na kujenga miundombinu mipya ya masoko na barabara pamoja na miundombinu ya huduma.

v. Kupunguza idadi na viwango vya tozo, ada na kodi za biashara na kuweka mfumo imara wa ufuatiliaji na tathmini ambapo Halmashauri itaendelea kupitia upya viwango mbalimbali vya tozo kulingana na hali ya uchumi.

vi. Kuendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara wadogo na wakati ili kuboresha biashara zao na kulipa tozo zinazotakiwa kwa wakati.

11.0 SEKTA YA MIFUGO

Katika kuzingatia ufugaji wa kisasa ifikapo 2025, Halmashauri itajikita kuboresha maeneo yafuatao:-

i. Kutoa mafunzo rejea kwa wafugaji na maafisa ugani kwa kushirikiana na sekta binafsi

ii. Kutoa chanjo kwa mifugo kwa kuzingatia mpango na ratiba ya chanjo

iii. Kuongeza miundombinu ya upatikanaji wa masoko ya mazao ya mifugo

12.0 SEKTA YA UVUVI

Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hii katika Halmashauri yetu tutaendelea kuhimiza uvuvi endelevu na wenye tija ifikapo kupitia maafisa uvuvi na vikundi vya usimamizi wa mialo ifikapo 2025, kwa kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuwaelimisha wavuvi umuhimu wa matumizi ya zana bora za uvuvi na kushirikiana na wananchi wema kupiga vita uvuvi haramu

ii. Kuanzisha mashamba darasa ya ufugaji wa samaki (fish carge) na mabwawa ili kuwawezesha ajira kwa vijana katika maeneo ya kata zilizomo ndani ya Halmashauri.

iii. Kuhamasisha wavuvi kujiunga katika vikundi na vyama vya ushirika vya msingi na kuongeza idadi ya vyama vya ushirika wa wavuvi kutoka 5 Mwaka 2020 hadi 10 Mwaka 2025

iv. Kuhamasisha Mashirika ya Umma na Sekta binafsi kuwekeza katika uanzishaji wa viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi pamoja na kuboresha masoko ya mazao ya uvuvi yaliyopo.

v. Kuhamasisha wananchi kuanzisha miradi ya ufugaji wa samaki, hii itaenda sambamba na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika uzalishaji wa vyakula vya samaki.

13.0 SEKTA YA KILIMO

Ili kuwa na kilimo cha mazao ya mbogamboga na chakula chenye tija ifikapo 2025, Halmashauri tutaendelea kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuhakikisha upatikanaji wa huduma na zana bora za kilimo cha kisasa.

ii. Kuwezesha wakulima kutumia mbinu za kisasa za kilimo endelevu na chenye tija.

iii. Kuhifadhi maeneo maalumu ya ukanda wa kijani ili kuongeza kilimo

cha mbogamboga.

iv. Kuimarisha miundombinu ya upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo kwa kuongeza idadi ya masoko kutoka 6 mwaka 2020 hadi 12 mwaka 2025

v. Kuendelea kuhimiza vijana kujiunga katika vikundi vya ushirika wa kilimo cha mazao ya bustani ili kuwawezesha kunufaika na mradi wa uwezeshaji toka ofisi ya waziri mkuu unaolenga kuchochea matumizi ya kitalu nyumba (green house).

14.0 SEKTA YA USHIRIKA

Katika kujenga ushirika kwa hiari ifikapo 2025. Ili kufanikisha lengo hilo, Halmashauri itafanya yafuatayo:-

i. Kuhamasisha makundi maalum kujiunga na kuanzisha vyama vya ushirika kutoka vyama 25 Mwaka 2020 hadi vyama 40 Mwaka 2025.

ii. Kuanzisha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOs) kwenye Ushirika wa Mazao na Masoko (AMCOS).

iii. Kuhimiza uanzishwaji wa vyama 15 imara vya ushirika vya msingi [halipimiki].

15.0 SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

Katika kuhakikisha wananchi wanawekewa mazingira mazuri ili washiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ifikapo 2025, Halmashauri itaendelea kutekeleza yafuatayo**:-**

i. Kuwezesha vijana, wanawake na makundi mengine ya wajasiriamali kujiajiri katika shughuli halali za kujipatia kipato ili kuongeza uzalishaji na kuinua uchumi wa Halmashauri.

ii. Kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kukuza kiwango cha kutoa mkopo wa 10% ya fedha zinazotolewa kwa vijana, wanawake na walemavu kutoka Tsh. 857,349,400.00 mwaka wa fedha 2020/2021 hadi Tsh. 1,300,000,000.00 ifikapo mwaka wa fedha 2024/2025

iii. Kuongeza utekelezaji wa miundombinu inayochochea ajira ili kuongeza fursa za ajira kwa vijana.

16.0 USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI KATIKA UWEKEZAJI

Katika kujenga sekta binafsi yenye mtizamo chanya wa kuwekeza katika viwanda ifikapo 2025, Halmashauri itaendelea kuchukua hatua zifuatazo:-

i. Kuhakikisha tunapanga na kupima ardhi kwa matumizi ya uwekezaji wa viwanda vidogo na vikubwa pamoja na matumizi mengine kama vile, mahoteli katika fukwe na kumbi za mikutano.

ii. Kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili uwekezaji.

iii. Tutaendelea kuondoa urasimu katika utoaji vibali na kufanya maboresho pale itakapobidi, ili kurahisisha upatikanaji wa vibali vya ujenzi viwe vinatolewa ndani ya siku saba za kazi.

iv. Halmashauri itahakikisha shughuli za ujenzi zinafanyika kwa kuzingatia taratibu, kanuni na sheria za ujenzi mijini. Hatutavumilia ujenzi holela usiozingatia taratibu za mipango miji.

IMC